JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
**CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI**

# TANGAZO LA KUWASILISHA MAOMBI YA KUISHI HOSTEL ZA NDANI YA CHUO



**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kinapenda kuwajulisha Wanafunzi wote kuwa, dirisha la maombi ya kuishi katika hosteli za Chuo kwa mwaka wa masomo 2026/2027 limefunguliwa.**

**Hivyo, Chuo kinawajulisha Wanafunzi wanaoendelea na masomo (continuing students) na Wanafunzi wapya (new entrants) wanaohitaji kuishi kwenye hosteli hizo wanapaswa kutuma maombi yao kuanzia tarehe 01/09/2026 hadi tarehe 10/10/2026 saa 23:59 usiku.**

**Utaratibu wa kutuma maombi kwa Wanafunzi wapya ni kama ifuatavyo:**

i. **Ingia kwenye tovuti ya Chuo https://sims.nit.ac.tz**

ii. **Kisha kwenye "username" ingiza "admission" namba yako, na kwenye "password" ingiza jina lako la mwisho (surname) kwa herufi kubwa.**

iii. **Bofya "Login"**

iv. **Bofya "Update Profile"**

v. **Bofya "Submission"**

vi. **Bofya "Submit Information"**

vii. **Baada ya hapo "profile" yako itabadilika. Hivyo, utabofya kwenye "accommodation", kisha kwenye "apply accommodation", utaendelea na hatua zinazofuata hadi mwisho na kutuma maombi yako.**

**Kwa Wanafunzi waliochaguliwa kutoka TAMISEMI watume maombi yao kwa kufuata utaratibu kama ilivyoelekezwa hapa chini:**

i. **Ingia kwenye tovuti ya Chuo https://www.nit.ac.tz**

ii. **Kisha kwenye "username" ingiza "admission" namba yako, na kwenye "password" ingiza jina lako la mwisho (surname) kwa herufi kubwa.**

iii. **Bofya "Update Profile"**

iv. **Bofya "Education Background"**

v. **Bofya "Add Academic Certificates"**

vi. **Jaza taarifa zako**

vii. **Bofya "Submission"**

viii. **Bofya "Submit Information"**

ix. **Baada ya hapo "profile" yako itabadilika. Hivyo, utabofya kwenye "accommodation", kisha kwenye "apply accommodation", utaendelea na hatua zinazofuata hadi mwisho na kutuma maombi yako.**

**Wanafunzi wanaoendelea na masomo wataingia kwenye *NIT-SIMS* kwa kutumia namba zao za usajili na "password" zao kisha kutuma maombi yao. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/10/2026 saa 23:59 usiku.**

**Aidha, taarifa za kina kuhusu hosteli hizo zimeorodheshwa katika Jedwali hapa chini.**

**Jedwali: Orodha ya Hosteli, aina ya Chumba na Bei zake**

| Na. | Jina la Hostel | Aina ya Chumba | Bei | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1 | WING "A" na WING "B" | *Self-contained* | 500,000/= | Mwaka |
| 2 | WING "A" na WING "B" | Kawaida | 300,000/= | Mwaka |
| 3 | Nyerere na Moringe | Kawaida | 250,000/= | Mwaka |

**NB: Kwa watakaokuwa wamekidhi vigezo na kuchaguliwa, malipo ya hosteli ni ya mwaka wa masomo husika ambayo yatafanyika kwa mkupuo (awamu moja tu) kupitia "control number" ambayo itapatikana kwenye akaunti ya Mwanafunzi, "Students' Information Management System" (SIMS).**

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kupitia Simu Namba +255 222 213 701/ 0788152 661 na Email: happiness.mremi@nit.ac.tz**

***Imetolewa na Ofisi ya Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi.***